HOTUBA YA UFUNGUZI WA MKUTANO WA WADAU WA UZINDUZI WA MPANGO WA KUONGEZA VIRUTUBISHI KWENYE UNGA WA MAHINDI MKOANI SONGWE

Tarehe: 29 Mei, 2018

Ndugu,
Wawakilishi kutoka Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,
Wawakilishi kutoka Shirika la viwango, Mamlaka ya chakula na dawa, Taasisi ya Chakula na LisheTanzania,
Wadau wetu wa Maendeleo toka USAID-NAFAKA,
Watendaji na Wataalam kutoka ngazi ya Mkoa na Halmashauri,
Wataalam kutoka Taasisi zisizo za Kiserikali,
Ndugu waandishi wa habari,
Mabibi na Mabwana,

Awali ya yote napenda nichukue fursa hii kuwakaribisha katika mkutano wa uzinduzi wa mpango wa uongezaji wa virutubishi kwenye unga wa mahindi. Aidha, poleni kwa safari na karibuni mkoani kwa wale wote mliotoka katika halmashauri zetu zilizo nje ya makao makuu ya mkoa wetu. Napenda pia kwa niaba ya uongozi mzima wa Mkoa wa Songwe kuishukuru Serikali yetu na wadau wetu USAID-NAFAKA kuwezesha mkutano huu. Kwetu sisi, hii ni heshima na fursa nyingine kubwa ya kutukutanisha pamoja viongozi na wataalam kutoka ngazi ya Mkoa na Halmashauri zote za Mkoa wetu kujadiliana kwa kina na hatimaye kuhakikisha mpango wa uongezaji wa virutubishi unafanikiwa kwa ajili ya kuboresha afya na lishe kwa jamii yetu.

Ndugu washiriki,
Urutubishaji wa chakula ni mojawapo ya njia zitakazosaidia kuboresha lishe na kuondoa matatizo yanayoambatana na lishe duni. Wataalam wanatuambia kuwa watoto waliopata huduma bora za lishe, hususani, katika kipindi cha siku 1,000 za kwanza za uhai wao, yaani tangu mama anapopata ujauzito hadi mtoto anapotimiza umri wa miaka miwili

wanapata faida zitakazodumu katika maisha yao yote. Baadhi ya faida hizo ni; maendeleo mazuri ya ukuaji wa ubongo, uwezo mzuri wa kukabiliana na maradhi, uwezo mzuri wa kiakili (higher IQ}, uwezo na ufanisi wa kujifunza na uwezo mkubwa wa kujiingizia kipato wakiwa watu wazima.

Ndugu washiriki,
Uwekezaji katika lishe pia unasaidia kuinua pato la Taifa kwa asilimia 2 hadi 3 kila mwaka. Aidha, wataalam wa uchumi wanatuambia kuwa utoaji wa vitamini na madini kwa watoto chini ya miaka mitano ni mkakati mzuri zaidi wa uwekezaji katika lishe. Kila dola moja ya Marekani ($1) inayowekezwa kwenye watoto kupitia mkakati huu utakuja kupata faida ya dola za Marekani thelathini ($30) hapo baadaye, hiki ni kiwango kikubwa kabisa cha faida katika uwezekaji wa aina yoyote.

Ndugu washiriki,
Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa kuwekeza katika lishe kama mkakati mmojawapo wa kufanikisha azma ya Serikali kufikia uchumi wa kipato cha kati na viwanda ifikapo 2025. Baraza la Umoja wa Mataifa limetoa azimio la kuwa kati ya mwaka 2016 hadi mwaka 2025 ni miaka ya "Kuchukua Hatua katika Kutekeleza Masuala ya Lishe - Decade of Action on Nutrition".

Ndugu washiriki,
Utapiamlo upo katika nchi nyingi duniani, lakini ni mkubwa zaidi katika nchi maskini na zinazoendelea ikiwemo Tanzania. Takwimu za hivi karibuni zimebaini kupungua kwa viwango vya kitaifa vya utapiamlo hasa kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka 5. Pamoja na kupungua kwa viwango hivi, bado inakadiriwa kuwa kuna zaidi ya watoto milioni 2.9 ambao wamedumaa nchini, 382,500 wana ukondefu na 106,000 wanaokabiliwa na utapiamlo mkali.

Ndugu washiriki,
Utafiti huu wa kitaifa umebaini kuwa hali ya lishe ya wanawake nayo bado ni mbaya nchini Tanzania. Asilimia 3 ya wanawake ni wafupi sana wakati asilimia 10 ni wembamba (asilimia 3 wana wembamba wa kadiri au ni wembamba sana-uwiano wa uzito na vimo vyao. Wanawake wenye utapiamlo wana uwezekano mkubwa wa kuzaa watoto wenye uzito pungufu na hivyo kurithisha utapiamlo kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Utafiti pia ulibaini kuwa kwa ujumla asilimia 45 ya wanawake walio katika umri wa kuzaa (miaka 15 ahdi 49) walionesha kuwa na upungufu wa damu, asilimia 30 walionesha kuwa na upungufu wa damu, asilimia 11 walionesha kuwa na upungufu wa kadiri wa damu na asilimia 1 walikuwa na upungufu mkubwa sana wa damu.

Ndugu washiriki,
Serikali inatambua kuwa bado zipo changamoto nyingi katika kukabiliana na utapiamlo hapa nchini. Pengine, changamoto kubwa kuliko yote ni ile ya uelewa mdogo wa masuala ya lishe katika jamii, kuanzia ngazi ya familia hadi kwa watendaji na viongozi wa Serikali. Uelewa mdogo kuhusu masuala ya lishe pia umesababisha masuala ya lishe kutopewa kipaumbele na kutofanikiwa katika utekelezaji ngazi za Halmashari, kata, vijiji na familia ambako ndiko waliko watoto na wanawake wengi wanaohitaji zaidi huduma bora za lishe.

Ndugu Washiriki;
Jambo la msingi ambalo sote tunapaswa kulifahamu ni kwamba lishe ni suala mtambuka na utapiamlo katika jamii ni matokeo ya mkusanyiko wa matatizo mengi ikiwa ni pamoja na ulaji duni usiokidhi viwango vya virutubishi vyote vinavyotakiwa katika mwili, maradhi mbalimbali, kutokuwa na uhakika wa chakula, matunzo duni ya wanawake na watoto, mazingira machafu na huduma duni za Afya, rasilimali haba na

mgawanyo usiokuwa na uwiano sahihi, umaskini wa kipato, siasa na hata sera zisizotambua umuhimu wa lishe kwa maendeleo ya nchi.

Ndugu washiriki,
Jambo jingine la msingi pia ambalo sote tunapaswa kulifahamu ni kwamba lishe duni kwa wanawake wajawazito inawaweka katika mazingira yanayoweza kusababisha kujifungua watoto njiti au kuharibu mimba. Lishe duni pia huwadhoofisha wanawake wajawazito na hivyo huugua mara kwa mara. Wengi wao hupata upungufu wa damu unaochangia kupoteza maisha wakati au baada ya kujifungua. Vifo vya wanawake wajawazito vitapungua sana endapo watakuwa na hali nzuri ya lishe katika kipindi chote cha ujauzito.

Ndugu washiriki,
Hivi sasa tunafahamu kwamba lishe bora katika siku 1,000 za kwanza za maisha ya mtoto, yaani tangu mimba inapotungwa mpaka motto anapotimiza miaka miwili. Hiki ndicho kipindi mtoto anapojenga msingi wa ukuaji wa mwili na maendeleo ya akili. Kwa bahati mbaya madhara ayapatayo mtoto katika ukuaji wake kimwili na maendeleo ya kiakili kutokana na lishe duni katika siku 1000 za kwanza za maisha yake hayawezi kurekebishwa kwa maisha yake yote.

Pia tunafahamu kuwa athari nyingine za lishe duni kwa mwanadamu ni pamoja na tezi la shingo (goita) kutokana na upungufu wa madini joto, upofu na kudhoofisha kinga ya mwili ambayo husababishwa na upungufu wa vitamin A, na upungufu wa damu ambao husababishwa na upungufu wa madini ya chuma. Upungufu wa asidi ya foliki husababisha wanawake wajawazito kuharibu mimba na kuzaa watoto wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi wakati upungufu wa vitamini C hupunguza uwezo wa mwili kutumia madini ya chuma na husababisha mtu kupata vidonda kinywani na fizi kutoka damu. Orodha ya athari za lishe duni ni ndefu, kwa leo itoshe kutaja hizi.

Ndugu washiriki,

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na utapiamlo nchini tangu tulipopata uhuru. Hatua hizo ni pamoja na uongezaji wa virutubishi kwenye unga wa ngano na wa mahindi mradi unaozinduliwa leo. Rai yangu kwenu ni kwamba fursa hii itumike vizuri. Tusikilize vizuri mada zitakazowasilishwa ili kupata mwanga zaidi kuhusu kile kinachoelezwa na kupendekezwa; msingi, mantiki, maudhui yake ili hatimaye kwa nafasi zetu tusaidie katika kutimia kwa malengo yaliyokusudiwa. Kila mmoja wetu, kwa nafasi yake ajitoe kwa dhati kuchangia kuleta hali bora ya lishe kwake, kwa familia yake na kwa Watanzania wote. Napenda kuwashukuru wadau wetu wa USAID-NAFAKA kwa jitihada zake inazochukua katika kutokomeza utapiamlo Tanzania kupitia programu yake ya kuongeza virutubishi hapa mkoani kwetu Songwe.

Waheshimiwa mabibi na mabwana baada ya kusema hayo; ***"NATAMKA RASMI KUWA MPANGO WA KUONGEZA VIRUTUBISHI UNAO RATIBIWA NA MRADI WA NAFAKA UMEZINDULIWA RASMI MKOANI SONGWE"***

Asanteni kwa kunisikiliza!

Chiku Galawa.
Mkuu wa Mkoa.
SONGWE.